

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA TISA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TISA

17 NOVEMBA, 2017

KIKAO CHA TISA – TAREHE 17 NOVEMBA, 2017

I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Tulia Ackson (Naibu Spika) alisoma Dua na kukiongoza Kikao cha Bunge.

Makatibu Mezani

1. Ndg. Ramadhan Abdallah
2. Ndg. Asia Minja

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Jenista Joakim Mhagama aliwasilisha Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 [*The Drug Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017*].

Mhe. Daniel Edward Mtuka aliwasilisha Maoni ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Mhe. Masoud Abdallah Salim aliwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 107: Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu

Nyongeza: Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu
Mhe. George Malima Lubeleje
Mhe. John Wegesa Heche

Swali Na. 108: Mhe. Margaret Simwanza Sitta

Nyongeza: Mhe. Margaret Simwanza Sitta

Swali Na. 109: Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo

Nyongeza: Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo
Mhe. Zacharia Paul Issaay

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na. 110: Mhe. John Wegesa Heche (kny: Mhe. Godbless
Jonathan Lema

Nyongeza: Mhe. John Wegesa Heche
Mhe. Ally Hassan Omar King
Mhe. Kunti Yusuph Majala
Mhe. Jaku Ayubu Hashim

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na. 111: Mhe. Hamidu Hassan Bobali

Nyongeza: Mhe. Hamidu Hassan Bobali
Mhe. Salma Rashid Kikwete
Mhe. Dunstan Luka Kitandula
Mhe. Joseph Roman Selasini

Swali Na. 112: Mhe. Zainab Athumani Katimba (kny: Mhe. Hasna
Sudi Katunda Mwilima

Nyongeza: Mhe. Zainab Athumani Katimba
Mhe. Zainab Matitu Vullu
Mhe. Maryam Salum Msabaha
Mhe. Abdallah Majula Bulembo

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 113: Mhe. Hawa Mchafu Chakoma

Nyongeza: Mhe. Hawa Mchafu Chakoma
Mhe Oliver Daniel Semuguruka
Mhe. Qambalo Willy Qulwi

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 114: Mhe. Nuru Awadh Bafadhili

Nyongeza: Mhe. Nuru Awadh Bafadhili
Mhe. Grace Sintando Kiwelu
Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi
Mhe. Omary Tebweta Mgumba

WIZARA YA NISHATI:

Swali Na. 115: Mhe. Omary Tebweta Mgumba

Nyongeza: Mhe. Omary Tebweta Mgumba
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde
Mhe. Hawa Subira Mwaifunga
Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Swali Na. 116: Mhe. Saed Ahmed Kubenea

Nyongeza: Mhe. Saed Ahmed Kubenea
Mhe. Khadija Nassir Ali

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Swali Na. 117: Mhe. Halima Abdallah Bulembo

Nyongeza: Mhe. Halima Abdallah Bulembo

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 118: Mhe. Kemirembe Julius Lwota

Nyongeza: Mhe. Kemirembe Julius Lwota

Swali Na. 119: Mhe. Cosato David Chumi (kwa niaba ya Mhe. Dkt. David Mathayo David)

Nyongeza: Mhe. Cosato David Chumi

Swali Na. 120: Mhe. Jesca David Kishoa

Nyongeza: Mhe. Jesca David Kishoa

VI. MATANGAZO

Wageni mbalimbali waliokuwa kwenye *gallery* za Bunge walitambulishwa Bungeni.

VII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Miswada ifuatayo ilisomwa kwa Mara ya Kwanza:-

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2017.

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2017.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Mwaka 2017.

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa Mwaka 2017 uliwasilishwa Bungeni na Mhe. Jenista Joakim Mhagama kwa Mara ya Pili.

Mhe. Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga alisoma Maoni ya Kamati kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Mhe. Masoud Abadallah Salim Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alisoma Maoni kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Baada ya uwasilishaji uchangiaji wa jumla ulifuata na wafuatao walichangia:-

- | | | |
|------------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Ally Saleh Ally | - | CUF |
| 2. Mhe. Mussa Bakari Mbarouk | - | CUF |
| 3. Mhe. Riziki Said Lulida | - | CUF |
| 4. Mhe. Ruth Hiyob Mollel | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Lucia Michael Mlowe | - | CHADEMA |
| 6. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab | - | CCM |
| 7. Mhe. Lucy Thomas Mayenga | - | CCM |

Naibu Waziri na Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu walihitimisha Hoja kwa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

V. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Bunge liliingia kwenye Kamati ya Bunge zima na wafuatao walichangia:-

- | | | |
|------------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab | - | CCM |
| 2. Mhe. Ruth Hiyob Mollel | - | CHADEMA |

Kamati ilimaliza shughuli zake na Bunge lilirudia na Waziri alitoa Hoja, Kamati na Bunge lilihojiwa na kuridhia Muswada husika.

Hapa Naibu Spika aliondoka na Spika aliingia na kuendesha Kikao.

VI. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

Katibu wa Bunge alitoa Taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwenye Mkutano huu zimekamilika.

VII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

Waziri Mkuu alitoa hotuba ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 30 Januari, 2018 na Bunge lilihojiwa na kuafikiwa.

VIII. TAARIFA YA SPIKA

Spika alitoa taarifa kuhusu masuala yafuatayo:-

1. Onyo kwa Wahariri wa Magazeti ya Mtanzania, Mwananchi, Nipashe kwa kosa la kuchapisha na kusambaza Mwendno wa Shauri lililokuwa likfanyiwa kazi na Kamati ya Maadili kuhusu Shauri la Mhe. Zitto Zuberi Kabwe kinyume na Kanuni za Bunge.
 - Wahariri waliomba radhi kwa kitendo hicho. Kamati ilishauri adhabu ya onyo kali na wachapishe kuomba radhi ndani ya siku tano vinginevyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali awapeleke Mahakamani.
2. Waraka wa Spika Na. 5/2017 – Kuunda Kamati Maalum ya ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu katika kuchangia Mapato ya Taifa. Kamati itafanya kazi kwa siku 30 kuanzia tarehe watakayoelezwa na Katibu wa Bunge na kuwasilisha Taarifa kwa Spika.
3. Waraka Na. 6/2017 – Kuunda Kamati Maalum ya ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Sekta ya Gesi. Kamati itafanya kazi kwa siku 30 kuanzia tarehe itakayojulishwa na Katibu wa Bunge na kuwasilisha Taarifa yake kwa Spika.

IX. MATANGAZO MENGINE

1. Mhe. Spika alitoa salamu za rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ndugu Yahya Msulwa aliyefariki duni jana usiku.
2. Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatafanyika tarehe 1 – 11 Desemba, 2017. Wabunge wote walihimizwa kuhudhuria.
3. Muswada wa kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu uletwe Bunge lijalo.

X. WIMBO WA TAIFA

Wimbo wa Taifa uliimbwa na Bunge liliahirishwa mpaka tarehe 30 Januari, 2017.